JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

**BODI YA CHAI TANZANIA**

---

# TAARIFA KWA UMMA

## KUJISHUGHULISHA NA BIASHARA YA CHAI (*TEA DEALERSHIP*) BILA KUWA NA LESENI KUTOKA BODI YA CHAI TANZANIA

Kwa mujibu wa Kanuni ya 20 ya Kanuni za Tasnia ya chai za Mwaka 2010 Mtu hataruhusiwa kutengeneza, kuchanganya na kufungasha chai kwa ajili ya kuuza isipokuwa kwa mujibu wa leseni inayotolewa na Bodi ya Chai Tanzania. Kujishughulisha na biashara ya chai bila kuwa na Leseni ni kinyume na Sheria ya Chai, Sura Na. 275.

3. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Kanuni ya 20 (1) atakuwa ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili lakini isiyozidi shilingi laki tano, au kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na mbili.

4. Kupitia tangazo hili, Bodi ya Chai Tanzania inapenda kutoa taarifa kwa Umma kwa kila mwananchi ajiepushe na uvunjivu wa Sheria ikiwepo kujihusisha na biashara ya chai bila kuwa na idhini kutoka Bodi ya Chai Tanzania.

Imetolewa na Bodi ya Chal Tanzania tarehe **03 Juni, 2025**

**MKURUGENZI MKUU**